# *NI NANI ANAWEZA KUWA MWANAFUNZI?*

## KIELELEZO CHENYE MSINGI JUU YA MAFUNZO YA YESU

***"Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli."* Yohana 8:31.**

***"Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu."* Yohana 15:7-8.**

***"Amri mpya nawapa, mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi nmpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wato watambue ya kuwa nyinyi mmekuwa wanafunzi wangu, Mkiwa na upendo nyinyi kwa nyinyi."* Yohana 13:34-35**

**Kimetayarishwa na Jean Manning**

# YALIYOMO

1. **Utangulizi – ni nani anaweza kuwa mwanafunzi?**
2. **Kudumu katika neno**
3. **Maombi yaliojibiwa – tunda la mwanafunzi**
4. **Kupenda/ kutumika kama vile yesu alivyopenda**
5. **Ni nini kinazuia mtu kuwa mwanafunzi?**
6. **Tabia na majukumu ya mwanafunzi**
7. **Kutumwa katika ulimwengu kama vile yesu alivyotumwa**
8. **Kutiwa nguvu kwa mwanafunzi**
9. **Maagizo Ya Mwanafunzi.**

### UTANGULIZI

# NI NANI ANAWEZA KUWA MWANAFUNZI?

Yesu alikuwa na wafuasi wengi. Wengine walikuwa wakistaajabu; wengine walimfuata wakitafuta miujiza; wengine walikuja kumtafutia makosa ndani yake; wengine walimfuata wakijua kuwa hakika yeye ni masihi. Wale waliomuamini wakawa wanafunzi wake.

## A. Yesu alisema mwanafunzi atajulikana kwa njia tatu tofauti.

- **Kudumu katika neno**
  ***"Basi yesu akawaambia wale wayahudi walioamwaamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli"* Yohana 8:31**

- **Maombi yaliyojibiwa**
  ***"Ninyi mikaa ndani yangu, na maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.* Yohana 15:7-8**

- **Kupenda /kutumika kama Yesu alivyo penda**
  **"*Amri mpya nawapa, mpendane kama vile nilivyo wapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambuua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.* Yohana 13:34-35**

## B. Yesu alitaja mambo matatu ambayo yanazuia mtu kuwa mwanafunzi.

Anapatiana maeneo matatu ambayo tunahitaji kupa kipa umbele katika maisha ya utiifu wetu kwake.

- **Katika uhusiano wetu na wengine Yesu ana nafasi ya kwanza**.
  **"*Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake wanaume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"* Luka 14:26.**

- **Katika njia yetu ya maisha Yesu ni lazima apewe nafasi ya kwanza**
  **"*Mtu ye yote asiye chukua msalaba wake na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"* Luka 14:27**

- **Mali yetu haistahili kutuzuia kumfuata yesu.**
  **"*Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"* Luka 14:33.**

# KUDUMU KATIKA NENO
# ISHARA YA MWANAFUNZI WA KWELI

**Kudumu katika neno ambayo Yesu alizungumzia ilikuwa ishara ya mwanafunzi wa kweli.**

Katika **Yohana 8:25-30** Yesu aliambia Wayahudi yeye ni nani "***Na alipo zungumza maneno hayo wengi wakamuani"***

Kwa waamini hawa akasema: ***"Nanyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli, tena mtafahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"*** **Yohana 8:31-32**. Lile neno ambalo Yesu alisema linaongea juu ya neno - lililo andikwa [*logos*].

Wakati neno linadumu ndani, ya mwanafunzi, ***"Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru."*** **Aya 32.**

## Kujua ukweli wa neno la Mungu*:*

- *Ina mwezesha mwanafunzi kutembea kwa imani katika utimilifu wa ahadi za Mungu.*
- *Inamwezesha mwanafunzi kuomba kwa ujasiri akitarajia jawabu za maombi yake Roho mtakatifu anapohuisha neno ndani yake.*

***"Nanyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lolote nanyi mtatendewa"*** **Yohana 15:7.** Neno hilo lililo huishwa huja kama matokeo ya neno lililo andikwa likihuishwa [*rhema*]

## NENO HUFANYA KAZI NAMNA GANI KATIKA MAISHA YA MWANAFUNZI?

- **Husafisha**
  **"*Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia."*** **Yohana 15:3**

- **Linatakasa**
  Neno la Mungu ni kweli na linatakasa mwanafunzi
  **"*Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ni diyo kweli"*** **Yohana 17:17.**

- **Linaleta mazao mazuri**
  Mwanafunzi ni mtu anaye soma na anayetayarisha moyo wake kulipokea neno. Neno likianguka katika moyo uliyo tayarika linatoa mazao mema.
  **"*Naye aliyepandwa penye udongo mzuri, huyu ndiye alisikiaye lile neno, na kuelewa nalo, yeye ndiye azaaye matunda, huyu mia, na huyu sitini, na huyu thelathini"*** **Mathayo 13:23.**

- **Baraka**
  Mwanafunzi hupokea Baraka kupitia kulisikia na kulitii neno la Mungu.
  ***"Lakini yeye alisema, Afadhali, heri waliosikia neno la Mungu na kulishika."*** **Luka 11:28**

- **Yaleta uhakika wa uzima wa milele**
  Yule asikiaye na kuamini ana uzima wa milele. Hatahukumiwa lakini amevuka toka mautini na kuingia uzimani.

“***Amin, amin, nawaambia, yeye alisikiaye neno na kuliamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini na kuingia uzimani”* Yohana 5:24**

- **Wale wamelisikia neno watahukumiwa nayale wametenda na neno.**
  “***Neno hilo nililo nena ndilo litakalo mhukumu”* Yohana 12:48.**

- **Kuandaa**
  Yesu awaita wanafunzi wake kukumbuka neno alilonena kwao, ili wawe tayari kwa yale yalio mbele.
  ***“Likumbukeni lile neno nililo waambia, Mtumwa si mkubwa kuliko Bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi nyinyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu”.* Yohana 15:20**

- **Kukumbusha**
  Mwanafunzi afaa kukumbuka yakuwa neno limetimizwa.
  ***“Lakini litimie lile neno lililo andikwa katika torati yao, Walinichukia bure”* Yoh 15:25**

- **Kuwafanya wengine kuamini**
  Ulimwengu utaamini kuwa Mungu alimtuma Yesu Kristo wakati wanafunzi wake (haswa wale wamechaguliwa kuwa mitume) wanazungumza neno.
  “***Wala sio hao tu ninawaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao”* Yohana 17:20.**

- **Kufanya kazi kikamilifu**
  Neno linafanya kazi kikamilifu kwa wale wameamini.
  “***Kwa sababu hiyo sisi nasi twashukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea sii kama neno la mwanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi ndani yenu ninyi mnaoamini”* 1 The 2:13.**

- **Kudhihirisha upendo wa Mungu**
  Upendo wa Mungu unakamilishwa katika neno lidumulo.
  “***Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli.”* 1Yohana 2:5.**

- **Kushinda**
  Neno lidumulo linamuwezesha mwanafunzi kumshinda Yule muovu.
  “***Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule muovu”* 1 Yohana 2:14** (**Pia Ufunuo 3:8-10**).

## MWANAFUNZI ATAFANYA NINI NA NENO?

- **Kunena neno bila kuogopa**
  “***…Na wengi wa hao walio katika Bwana, hali wakipata kuthibitika kwa ajiri ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kulinena neno la Mungu pasipo hofu”* Waphilipi 1:14**

- **Kulishika sana neno la uzima**
  “***Mkishika sana neno la uzima; nipate sababu yakuona fahari katika siku ya Kristo, yakuwa sikupiga mbio bure wala sikujitaabisha bure”* Waphilipi 2:16.**

- **Kutumia kwa halali neno la kweli**
  **"*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli"* 2 Tim 2:15**

- **Hubiri neno**
  **Neno la Mungu hudhihirishwa kupitia kuhubiriwa.**
  **"*Akalifunua neno lake kwa majira yake katika ule ujumbe…"* Tito 1:3**

  ***"Lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usio kufaa, karipia, kemea na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho"* 2 Tim 4:2.**

**Yesu alisema kwa wale walio mwamini,**

**"*Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli.***

***Tena mtafaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru."***
**Yohana 8:31-32**

# MAOMBI YALIYO JIBIWA
# TUNDA LA MWANAFUNZI

***“Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa”.***

***“Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana, nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.”* Yohana 5:7-8**

Yesu alisema maombi yaliyojibiwa ni ishara ya uwanafunzi. Zinaonyesha kuwa mwanafunzi ana mazao. Anaongezea yakuwa mwanafunzi atampa Mungu utukufu kwa matunda haya.

## MWANAFUNZI ANAWEZAJE KUWA NA MAZAO KATIKA MAOMBI?

- **Kudumu katika neno**

  Yesu ameweka hii kuwa masharti ya mwanafuzi kupokea jawabu za maombi. “***Mkiomba neno lote kwa jina langu, hilo nitalifanya”* Yohana 14:14.**

  Mwanafunzi anapojua neno la Mungu, anaweza kuomba na kukubaliana na neno la Mungu ambalo lina huishwa kwa mawazo yake, na hivyo kuyaomba mapenzi ya Mungu yatendwe ulimwenguni

- **Kutumia muda katika uhusiano na Mungu Baba**

  Yesu aliwatangazia sababu gani yeye alitumia muda mwingi kwa maombi. Alijua la kufanya kwa kuwa alikuwa na Baba katika maombi.

  “***Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote atendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile.”* Yohana 5:19**

  ***“Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake yeye aliye nipeleka”* Yohana 5:30**

  Yesu aliwakumbusha yakuwa “***Yatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake”* Mt 10:25a**

- **Kwa kutambua kuwa enzi ni pahali pa maombi – pahari pa mamlaka**

  Mamlaka yote yatiririka kutoka kwenye enzi, ambapo Yesu ameketi. Mungu amemuinua Yesu kutoka kwa wafu na kumketisha “***Juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na ushultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia. Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake akamuweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajiri ya kanisa”* Eph 1:20-22**.

  Mwanafunzi Yule ambaye amefufuliwa pamoja na Kristo ameketishwa pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho **Eph2:6,** astahili ayatafute mapenzi ya Baba mbinguni na aombe mapenzi ya Mungu yatendeke hapa ulimwenguni.

  Mwanafunzi anapoweka mawazo yake kwa mambo yaliyo juu **Kol 3:1-2** Yuapaswa kuomba: ***Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni”* Mt 6:19.**

- **Kwa kuomba kama vile Yesu alivyo tufunza**

  Wakati wanafunzi walimuuliza Yesu awafunze kuomba. **Luka 11:1** aliwafunza, ***"Basi ninyi salini hivi"*** **Mt 6:9-13**.

  Waamini wameomba kwa 'muundo' huu ombi (lijulikanalo kama ombi la Bwana kwa waamini wengi) daima na hawajatambua yakuwa Yesu aliipatiana kwa wanafunzi wake kwa maana wanafunzi wake walimuuliza **awafunze kuomba.** Aliipatiana kwa wanafunzi wake kufunza mambo ya mbele wanapokuja kwake kwa njia ya maombi.

### Ombi hili ni la uhusiano

- Tunatambua sehemu yetu kama wana wa Baba kupitia Yesu Kristo;
- Tunatambua na kufahamu uhusiano wetu na waamini wenzetu ambao pia huongea na Mungu **"Baba yetu"**

Katika muundo huu wa maombi Yesu anafundisha kuwa maombi yanaingiwa kupitia ibada ya Mungu mwenyezi ambaye anatamalaki milele na ambaye twamtegemea.

- Ambaye hutoa mkate wetu wa kila siku – wa kimwili na wa kiroho
- Ambaye anatusamehe na kutukumbusha juu ya umuhimu wa kuwasamehe wengine.
- Ambaye anatulinda na kutuweka kutoka kwa yule muovu.

Mwanafunzi anayeomba '**kwa njia hii**' atatembea kwa ahadi za Mungu.

- Kwa **kusikiza** na kuona mapenzi ya Mungu katika kila hali.
  ***"Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni"*** **Mathayo 26:41, Mariko 14:38, Luka 22:40, 46**
  Yesu aliweka mfano. Yote aliyoyatenda ilikuwa ni matokeo ya kusikia kutoka kwa Baba.
  ***"Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba akitenda"*** **Yohana 5:19**

- Aliwaambia wanafunzi wake, **waulize katika maombi, wakiamini**
  **"*Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote muombao mkisali, aminini kwamba mmeyapokea, nayo yatakuwa yenu"*** **Mariko 11:24**

- Aliwaambia umuhimu wa **kuwaombea wafanyi kazi**
  **"*Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake"*** **Mt 9:38.**

- **Kesha na uombe**
  Yesu aliwaambia yakuwa yule atakesha na kuomba atahesabiwa amestahili kuepuka majaribu yatokayo juu ya ulimwengu.
  ***"Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika hayo yote yatakayotokea, na kusimama mbele ya Mwana wa Adamu"*** **Luka 21:36.**

- **Kustahimili katika maombi**
  ***"Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu siku zote, wala wasikate tama"*** **Luka 18:1.**

## NYUMBA YA MAOMBI

### Mwili huu ni hekalu ya Roho Mtakatifu

Paulo anazungumzia kanisa kama hekalu ya Mungu.

***"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi".*** **1 Kor3:16-17**

Wanafunzi wanajengwa kama makao ya Mungu katika Roho.

***"Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote limeungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye nanyi mmejengwa kuwa maskani ya Mungu katika Roho"*** **Efe 2:20-22.**

Katika maisha yake ulimwenguni, Yesu alienda katika hekalu la Mungu ulimwenguni na kulitakasa. Alitupa nje kila mazoea ya mwanadamu yaliyokuwa yameongezwa katika mwelekeo ambao Mungu aliwapatia kupitia. (**Mt 21:12-16)**

Alinukuru kutoka cha nabii **Isaya 56:7 "*Kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya pango la wanyang'anyi"* Mt 21:13**

Yesu alitakasa hekalu kuwa nyumba ya maombi na mara tu nguvu zikaachiliwa katika nyumba na vipofu wakaona na viwete wakatembea **(aya 14)**

Vipofu na viwete ni wale ambao ufahamu wao wa neno la Mungu ulikuwa umepungukiwa kwa sababu ya tabia za dhambi katika hekalu na mwenedo wao na Mungu ulikuwa umepotoka

Maombi yakisha rejeshwa hekaluni, vikwazo vinaondolewa na nguvu inaachiliwa kwa uponyaji. Kisha kukawa na furaha na sifa **(aya 15)**

Hekalu (mwili wa waamini) nilazima utakaswe kutokana na dhambi ili kuwe na njia safi ya maombi kwa Baba.

- **Mungu hujibu maombi ya imani**
- **Nguvu zinaachiliwa**
- **Neno la Mungu linadhihirishwa**
- **Mungu anatukuzwa**

### Neno la Mungu linapodumu ndani:

1. Mwanafunzi ataomba katika utiifu na kukubaliana na mapenzi ya Mungu.
   Yesu alisema: ***"Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani kwa neno lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni"*** **Mt.18:19**

2. Nguvu zitaachiliwa na kutakuwa na furaha kubwa katika kanisa la Mungu na Mungu atatukuzwa.
   Yesu alisema: ***"Amin, amin, nawaambieni, yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, kubwa kuliko hizo atazifanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba"***

***"Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lolote kwa jina langu nitalifanya"* Yohana 14:12-14.**

"Ninyi mkikaa ndani yangu,
na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni
Mtakalo lote nanyi mtatendewa.

"Hivyo hutukuzwa Baba yangu
Kwa vile mzaavyo sana;
Nanyi mtakuwa wanafunzi wangu."
Yohana 15:7-8

# KUPENDA NA KUTUMIKA KAMA YESU ALIVYOPENDA ISHARA YA MWANAFUNZI WA KWELI.

***"Tazama mtumishi wangu nimtengemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye; nimetia Roho yangu juu yake."*** **Isaya 42:1-2**

- **Mungu alijinyenyekesha**
- **Na akaja ulimwenguni kwa mfano wa mtu**
- **Kutumikia wanadamu kama Mwana wa Mungu.**

Mungu alifanya hivi kwa upendo wake mkuu kwa vyote alivyoviumba.

***"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele".*** **Yohana 3:16.**

### Jina Lake ni Yesu

Katika mfano wa mwanadamu kama Mwana wa Mungu, Yesu alifanyika mtumishi kwa wanafunzi wake na akawaosha miguu yao.

### Aliuweka mfano

**"*Ninyi mwaniita, mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vyema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi niliye Bwana na mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwakuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyotenda, ninyi mtende vivyo"*** **Yohana 13:13-15**.

### Alipeana amri mpya

Katika mazingira ya kutawadha uchafu wa barabara kutoka miguu ya wanafunzi wake, Yesu alipeana amri mpya kwa wanafunzi wake: "***Mpendane kama vile nilivyowapenda ninyi"*** **Yohana 13:34.**

Yesu alitangaza haya – upendo unaoelekeza kwa utumishi – kuwa ishara ya mwanafunzi: **"*Hivyo watu wote watatambua kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi"*** **(aya 35)**

Yohana anaweka wazi mambo matatu ambayo Yesu alikuwa na uhakika wake alipo dhihirisha upendo wake kwa wanafunzi kwa kuwatawadha wanafunzi miguu.
Wakati Yesu aliwaambia wapendane kama vile alivyowapenda, alitaka wanafunzi wake wahakikishiwe sehemu yao na Mungu katika maeneo hayo hayo.

**YESU ALIJUWA NINI?**
**"Yesu**

1. ***Akijuwa yakuwa Baba amepatiana vitu vyote mikononi mwake,***
2. ***na yakuwa alikuwa ametoka kwa Mungu***
3. ***na alikuwa anaenda kwa Mungu***

***aliondoka chakulani; akaweka kando mavazi yake, akatwaa kitambaa, akajifunga kiunoni. Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga"*** **Yohana 13:3-5.**

1. **Yesu alijua yakuwa Baba aliviweka vitu vyote chini ya mikono yake**
    - **Alikuwa ni Mungu mfano wa mwanadamu**

Kabla ya Yesu kuja hapa ulimwenguni, alikuwa na mfano wa Mungu ***"Kristo Yesu alikuwa yuna namna ya Mungu"*** **Flp 2:6.**

Alikuja ulimwenguni kwa mfano wa mtu kama Mwana: ***"Alipoonekana ana umbo kama mwanadamu"*** **Flp 2:8.**

Alitangazwa na Mungu katika ubatizo wake: ***"huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye"*** **Mt 3:17.**

- **Yeye ndiye mridhi wa vyote**

***"Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote,"*** **Ebr 1:1-2**

- **Alikuwa na mamlaka ya Mungu.**

**"*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"*** **Mt 28:18.**

- **Alikuwa muumba wa vyote**

***"Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika"*** **Yohana 1:3**

2. **Yesu alijua alikotoka**

Alifanyika kwa Roho wa Mungu.

***"Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukuwa Miriamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu"*** **Mt 1:20.**

3. **Yesu alijua alipokuwa akienda.**

***"Naenda kuwaandalia mahali" Yohana 14:2.***

**Akijua mambo hayo matatu – Mwana alifanyika mtumishi:** ***"Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu"*** **Flp 2:7**

**Kanisa, lililofanywa na wanafunzi, latakikana kuwa na mawazo yale aliokuwa nayo Yesu – kufahamu alicho kifahamu Yesu.**

Katika waraka wake kwa Wafilipi, Mtume Paulo, analihimiza kanisa pale linapaswa kuwa kama Yesu.

***"Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu. Ambaye mwanzo alikuwa ana namna ya Mungu, Naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, Akawa ana mfano wa mwanadamu, tena alipoonekana na umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, Naam, mauti ya msalaba". Flp 2:5-8.***

## Yesu ameweka vitu vyote mikononi mwa wanafunzi wake

Kama mtumishi, **Yesu aliweka mfano** Kwa wanafunzi wake waifuate. Ameweka vitu vyote mikononi mwa wanafunzi wake. Amepeana vipawa (**Warumi 12:6)** Kwa wanafunzi kutambua na kufahamu.

- **Yesu ameacha kanisa** mikononi mwa wanafunzi "***Mitume, manabii, wainjiristi, wachungaji na walimu"* Efe 4:11**

- Alipatiana **funguo za ufalme** kwa Petro, ambaye alikuwa na imani ndani ya Yesu, kama Masihi "***Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbiguni"* Mt16:19**

- Aliongea kwa mafumbo ya **Majukumu** yatakayokuja

"***Ninani basi Yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake alimuweka juu ya nyumba yake, awape watu wake chakula kwa wakati wake"* Mt 24:45**

***"Maana ufalme wa mbinguni ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake"* Mt 25:14**

- Yesu aliwapa **Mamlaka** wanafunzi wake

**"*Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru"* Luka 10:19**

- **Amewapa nguvu** wanafunzi kwa kumtuma Roho Mtakatifu kudumu ndani yao

***"Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini hata mvikwe uwezo utokao juu"* Luka 24:49.**

## Mwanafunzi anajua mianzo yake ya kiroho

***"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake, Waliozaliwa, si kwa damu, wala kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu"* Yohana 1:12-13.**

Kuzaliwa kwetu kiroho, ujuzi wetu wa 'kuzaliwa mara ya pili' ni kutoka kwa Mungu (**Yohana 3:3-6)** na ni "***sawasawa na Uradhi wa mapenzi yake"* Efe 1:5**

## Mwanafunzi anaijua hatima yake ya milele

***"Basi mimi nikienda na kuwaandali mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo"* Yohana 14:3**

Yesu ameandaa mahali petu ili tuwe naye milele. Pahali petu pa kudumu milele ni kama "***Mrithi wa Mungu"* Wagaratia 4:7.**

Yesu anatawala na kutamalaki milele na Mungu ***"Ametufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu"* Efe 2:6**

- Sio bidii mwanafunzi akitumika akiwa na uhakika huu. **Halleluyah!**

## Penda kama nilivyokupenda

Mtume Yohana, alilihimiza kanisa katika waraka wake kutii amri ambazo Yesu aliwapatia wanafunzi wake katika **Yohana 13:34-35.** Waraka wake ulihimiza waamini kwa nguvu kupenda kama Yesu alivyopenda.

- "***Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, maana hii ndiyo habari mliyoisikia tangu mwanzo, kwamba tupendane sisi kwa sisi"* 1Yohana 3:10-11.**

- ***"Yeye asiyependa, akaa katika mauti"* 1 Yohana 3:14.**

- "***Na hii ndiyo amri yake, kwamba tuliamini jina la Mwana wake Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi, kama alivyotupa amri"* 1 Yohana 3:23**

- "***Wapenzi, na tupendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na Kila apendaye ametoka kwa Mungu, naye anamjua Mungu."***
  ***"Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maaana Mungu ni upendo"***
  ***"Katika hili pendo la Mungu linaonekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwana pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye"***
  ***"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwana kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu"***
  ***"Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa sisi kupendana"***
  **1 Yohana 4:7-11.**

Yesu aliwafunza wanafunzi wake na kuwatuma ulimwenguni kama vile alivyotumwa. Mungu alijinyeyekeza, akaja ulimwenguni kwa mfano wa mwanadamu kama Mwana wa Mungu, na kuwaokoa wanadamu.

Mwanafunzi aliye komaa, akijua msimamo wake kama mwana wa Mungu, hujinyeyekeza na kuwatumikia watu na upendo ambao Yesu alionyesha.

Yesu alijua kwamba yuko ulimwenguni
Kumdhihirisha Mungu kikamilifu,
Upendo wake,
Na ufalme wake kwa wanadamu.

### Alikuja kutimiza unabii

**"*Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye"* Isaya 42:1**.

### Alikuja kama mtume wa Mungu

***"Mtafakarini sana Mtume na kuhani mkuu wa maungamo yetu"* Waebrania 3:1.**

Alisema: "***Aliye niona mimi amemuona Baba"* Yohana 14:9.**

Ujumbe wake ulikuwa ni wa kiufalme ukitoka kwa mfalme.
"***Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia"* Mt 4:17**

### Alikuja na mamlaka ya Mungu na ufalme wake

**"*Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"* Mt 28:18**

### Mwana alifanyika mtumishi

Yesu: "***Hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana"* Wafilipi 2:6, *"bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu"* Wafilipi 2:7.**

Mwanafunzi anatembea kama mwana aliyekomaa wa Mungu na mridhi pamoja na Kristo **Warumi 8:16-17** akijua, ***"Mungu, wa Baba wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa Baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo"* (Efe 1:3)**

Bali Yesu anatukumbusha: ***“Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu na yeyote atakayejikweza, atadhiliwa; na yeyote atakayejidhili atakwezwa”*** **Mt 23:11-12.**

***“Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwemo ndani ya Kristo Yesu”***
**Wafilipi 2:5**

***“Mpendane kama vile nilivyo wapenda ninyi”*** **Yohana 13:34.**

***“Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi” aya 35.***

# NI NINI KINAZUIA MTU KUWA MWANAFUNZI?

Yesu alisema mambo matatu ambayo yanaweza zuia mtu kuwa mwanafuzi. Anapatiana maeneo matatu ambayo yanaleta kipaumbele na utiifu wetu kwake.

1. Katika **uhusiano** na wengine Yesu ana nafasi ya kwanza
   "***Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe hawezi kuwa mwanafunzi wangu"*** **Luka 14:26**

2. Katika **maisha yetu** Yesu ni lazima apewe nafasi ya kwanza
   *"**Mtu yeyote asiyechukua msalaba wake na kunifuata na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"*** **Luka 14:27**

3. **Mali** yetu haistahili kutuvuta nyuma katika kumfuata Yesu
   **"*Basi, kadhalika, kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"*** **Luke 14:33**

*Wakati Yesu amepewa nafasi ya kwanza katika maisha ya mwanafunzi kila uhusiano zingine zanaingia katika mpango.*

### Yesu ni wa kwanza

- Yesu ana sehemu ya kwanza katika uhusiano wetu wa kijamii
- Yesu ana sehemu ya kwanza katika huduma ambayo mwanafunzi amepewa
- Yesu ana sehemu ya kwanza katika kanisa

**"*Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikamana katika yeye, Naye ndiye kichwa cha mwili wake, yaani cha kanisa, naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote, Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza utimilifu wote ukae"*** **Wakolosai 1:17-19**

### Yesu aliwaita wanafunzi wake

- **Walimfuata**

Yesu alipowaita wanafunzi wa kwanza, Simioni, aliyeitwa Petro na Andelea ndugu yake kumfuata, twasoma ***"Mara Wakaziacha nyavu zao na kumfuaata"*** **Mt 4:20**

***"Akaendelea mbele, akaona ndugu wengine wawili, Yakobo wa Zabedayo, na Yohana nduguye, ambao walikuwemo chomboni pamoja na Zebedayo baba yao, wakizitengeneza nyavu zao; akawaita. Mara wakakiacha chombo na baba yao, wakamfuata"*** **Mt 4:21-22.**

- **Wakaviacha vyote**

Katika mwisho wa siku zake ulimwenguni, wanafunzi hawa walimkumbusha Yesu yakuwa walikuwa wameviwacha vyote wamfuaate yeye ***"Tazama, sisi tumeacha vyote tukufuate wewe"*** **Mariko 10:28.**

- **Yesu anadhawabu**

***"Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba na watoto, au mashamba, kwa ajili yangu na kwa ajili ya injiri, ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele"*** **Mariko 10:29-30**

Yesu anawakumbusha wanafunzi wake yakuwa dhawabu za kiroho zimeshida Baraka za kiasiri/mwili. Kuna jamii ya kiroho na uridhi wa kiroho ambayo ni zaidi ya yale mwanadamu anaweza kudhania.

## YESU ANA NAFASI YA KWANZA

### 1) Katika uhusiano wetu na wengine

***"Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"*** **Luke 14:26**

Aya hii nivyepesi kuifahamu ukitambua ya kuwa neno **chukia = mbila upendo**

Uhusiano wa kiasiri wa kijamii unaboreshwa wakati Yesu anatambuliwa kwanza. Anaelekeza kwa hekima na ubabanuzi ambao unaleta kuitikia kwa hari kuliko kuharibu kwa hari

✓ **<u>Uhusiano wa kijamii ni wa muhimu kwa Yesu</u>**

**a) Ndoa ni sehemu ya makusudi ya Mungu kwa mtu**

Aliamua kuchagua kumpa Adamu msaidizi.

***"Bwana Mungu akasema, si vyema mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye"*** **Mwanzo 2:18**

**b) Watoto ni dhawabu kutoka kwa Mungu**

***"Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, Uzao wa tumbo ni thawabu"*** **Zaburi 127:3**

**c) Wazazi ni lazima watunzwe na washughulikiwe**

***"Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako" Kutoka 20:12.***

Yesu aliwakemea Waandishi na Mafarisayo katika hari ya kuto lishughulikia jambo hili vyema. (**Mt 15:4-6).** Yesu alionyesha umuhimu wa sheria hii alipo ongea msalabani na kumweka mama yake chini ya uangalizi wa mwanafunzi wake aliyempenda.

***"Basi Yesu alipomwona mama yake, na yule mwanafunzi aliye mpenda amesimama karibu, alimwambia mama yake, mama, tazama, mwanao, Kisha akamwambia yule mwanafunzi, tazama, mama yako. Na tangu saa ile mwanafunzi yule akamchukuwa nyumbani kwake"*** **Yohana 19:26-27.**

**d) Ushirikiano wa kijamii ni lazima udumishwe kanisani**

Mtume, Paulo, anaandikia, watoto, wakina baba, watumishi katika **Waefeso 6:1-8** na kukumbusha kanisa **Aya 8** ***"Mkijua ya kuwa kila neno jema alitendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana, kwamba ni mtumwa au kwamba ni huru"***

Wakati Yesu Kristo amepewa nafasi ya kwanza katika kila uhusiano – Nyumbani, Katika Kanisa, Kazini – mwanafunzi atakwenda nuruni ***"Bali tukienda nuruni, kama vile yeye***

***ako katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake yatuosha dhambi yote"*** **1Yohana 1:7.**
***"Na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo"*** **1Yohana 1:3a**

2) **Katika njia Yetu ya maisha Yesu nilazima apewe nafasi ya kwanza.**

***"Mtu yeyote asiye uchukua msalaba wake nakuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"*** **Luka 14:27**

Wakati Yesu alipouchukua msalaba wake, alikufa na akafufuka tena katika ufufuo. Vivyo hivyo anatarajia wanafunzi wake kufa ili wamwishie Kristo. Kufuatia kifo hiki kuna maisha ya ufufuo kwa waamini katika Roho.

Mtume Paulo alisema ***"Nimesulubiwa Pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala simimi tena, bali Kristo yuhai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajiri yangu."*** **Wagalatia 2:20.**

**Awezaje mtu kufa?**

a) **Kwa imani.**

Mwanafunzi atembea kwa imani akiamini kile Yesu amekamilisha msalabani. Kuna mabadiliko yanayotokea msalabani – Yesu alichukua dhambi zetu na akatupatia uhai wake.
***"Yeye asiye jua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajiri yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."*** **2 kor 5:21.**

Kwa imani mwanafunzi anapokea uzima huu mpya ***"Tukijua neno hili, yakuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye"*** **Warumi 6:6.**

b) **Kupitia ubatizo**

Mara tu mwanafunzi anapobatizwa kwa kumpokea Yesu, kwa imani anapokea uzima mpya. Mwanafunzi anaamini ***"Sisi sote tulio batizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyo fufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."*** **Warumi 6:3-4.**

***"Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini yakuwa tutaishi pamoja naye."*** **Warumi 6:8**

c) **Kwakutembea katika Roho**

Maisha mapya ni maisha ya kiroho katika mwili wa mwanadamu. ***"Basi nasema, enedeni kwa Roho wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili"*** **Wagalatia 5:16**

Paulo anaorodhesha ***"matendo ya mwili"*** **Gal 5:19-21** na anamkumbusha mwanafunzi ***"Na hao walio na KristoYesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake"*** **Gal 5:24.** Anasema ***"Tukiishi kwa Roho na tuenede kwa Roho"*** **Aya 25.**

d) **Kwa kukabiliana na dhambi**

Somo katika **Kol 3:5-15 I**nathihirisha kwamba kuna mambo ya mwili tustahiliyo ***'kuyavua'*** na utu upya ***'mkivaa'*** (**aya 10**).

***"Basi vifisheni viungo vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tama mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndio ibada ya sanamu"*** **aya 5.**

Kuna jukumu la mwanafunzi kukabiliana na maaisha ya mwili. ***“Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake”*** **Aya 8-9**

***“Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumulaum mwenzake; kama Bwana alivyo wasamehe ninyi, vivyo hivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu.”*** **Kol 3:12-14**

**e) Kwa kufanywa upya katika maarifa**

Mwanafunzi ni mtu mpya anabadirishwa kwa mfano wa Kristo **Warumi 8:29.** Kwa hivyo mwanafunzi ni lazima: ***“Avae utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake aliyemuumba”*** **Wakolosai 3:10**

Huyu mtu mpya ata ***“Atafikiria yaliyo juu, sio yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu”*** **Wakolosai 3:2.**

Mwanafunzi atabadirishwa kwa kufanywa upya mawazo yake ili ajue ***“Mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kupendeza, na ukamilifu.”*** **Warumi 12:2**

**Mwanafunzi ambaye amechukua msalaba wake’ kumfuata Yesu atajikana mwenyewe na atatembea ndani ya Roho akidhihirisha Yesu na ufalme wa Mungu duniani.**

### 3) Mali yetu haistahili kutuzuia kumfuata Yesu

***“Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu”*** **Luka 14:33.**

Katika mfano wa mpanzi, Yesu anaonya yakuwa “***Shughuli za dunia na undanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neno likawa halizai”*** **Mariko 4:19.**

Yesu anaonya nia ya mawazo ya mtu kuhusiana na mali.

- Yesu alieleza mfano wa mfalme ambaye aliwaalika watu katika karamu ya harusi ya mwanawe **Mt 22:2-12.** Ni fursa ya ajabu namna gani kualikwa kwa sherehe kama hii! Lakini watu walikataa mwaliko kwa maana walitilia maanani umuhimu mkuu kwa mali zao na kazi zilizo hitajika kufanywa kuhifadhi mali hiyo.
  ***“Lakini hawakujali, wakaenda zao, mmoja shambani kwake, mmoja kwenye biashara yake”*** **Mathayo 22:5**

- Wakati Yesu alizungumza na yule mtawala aliyetaka kumiliki uzima wa milele aliona moyo wa mtu aliyeweka sheria lakini akaweka umuhimu mkubwa kwa mali yake.
  Yesu alimwambia ***“Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha joo unifuate. Walakini yeye akakuja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi”*** **Mariko 10:21-22.**
  Yesu akaona huzuni yake kwa kufikilia vile ataachana na mali yake na akasema; ***“Jinsi itakavyo kuwa shida mweye mali kuingia katika ufalme wa Mungu”*** **aya 23.**

Wanafunzi walishangaa kwa maneno haya **Mariko 10:28-30.** Lakini Yesu akawakumbusha wanafunzi yakwaba dhawabu za kiroho zimeshinda dhawabu za kimwili.

## Mwanafunzi anafanya nini na mali yake?

**I.** Twaona katika injili yakuwa kulikuwa na wanafunzi ambao walikuwa mawakili wazuri wa mali waliyokuwa nayo walitumia mali zao kusaidia Yesu na wanafunzi.
Maria, Martha na Lazaro walikuwa wakarimu kwa Yesu marafiki wake huko Bethania.

**a)** ***"Basi wakamwaandalia karamu huku"*** **Yohana 12:2**

**b)** ***"Na Yohana mkewe kuza, wakili wake Herode, na Susana, na wengine wengi, waliokua wakimhudumia kwa mali zao".*** **Luka 8:3**

**c)** ***"Yusufu wa Arimathaya, mtu tajiri aliyekuwa mwanafunzi wa Yesu, akautwaa mwili wa Yesu na akauweka kwenye kaburi lake jipya"*** **Mathayo 27:57-60**

**II.** Katika kitabu cha **matendo ya mitume** twasoma. "***Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote walikuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta dhamani ya vile vitu vilivyouzwa, wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji"*** **Mdo 4:34-35.**

***"Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika. Wakiuza mali zao, na vitu vyao, walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na hitaji"*** **Mdo 2:44-45**

**III.** Katika **nyalaka**, Twaona makanisa ambayo yalikuwa na uwezo wa, kutuma msaada kusaidia sehemu ya mwili waliokuwa na ukame na kiangazi. Paulo anasafiri kutoka Makedonia na Akaya kufanya ***"changizo kwa ajiri ya watakatifu huko Yerusalemu walio maskini"*** **Warumi 15:26.**

Paulo anapongeza kanisa la Philipi kwa kushiriki kwa masumbuko yake. ***"Kwa kuwa hata huko Thesalonike mliniletea msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja."*** Anaongea juu ya ***"Mazao yanayozidi kuwa mengi katika hesabu yenu"*** **Wafiphilipi 4:16-17**

Paulo anaongea kuhusu vipawa zilizo patianwa na kanisa moja kwa lingine***"Tunayo itumikia, ili Bwana atukuzwe, ikadhilike utayari wetu"*** **2 Kor 8:19**

Himizo lake linamkumbusha mwanafunzi:

- Kuwa na mawazo ambayo ni tayari
- Yakuwa kutoa ya namna hii humletea Mungu utukufu.

## Yesu alionaje kuhusu mali?

Katika ujumbe wa Mlimani Yesu anawaonya wanafunzi wake ***"Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusipoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wale wevi hawavunji wala hawaibi. Kwakuwa hazina yako ilipo ndipo utakapokuwepo na moyo wako."*** **Mt 6:19-21**

Anachofanya mwanafunzi na mali yake, chaonyesha nia ya moyo wake. Yesu anatambua mahitaji ya mtu na tamaa zake. Mahubiri yake yanafundisha mtu njia bora ya kuangalia mali, **Mt 6:25-34.**

**Yesu akawaamuru wanafunzi:**
***"Bali utafuteni ufalme wake, na haki yake;***
***na hayo yote mtazidishiwa"*** **Mt 6:33**

# TABIA ZA MWANAFUNZI

Katika injiri zote nne mfano wa tabia kwa wale waliofanyika wanafunzi (wajifunzao) kama vile walitembea na kuishi na Yesu. Tunaona wakikomaa kwa kumpokea Yesu na kwa mambo aliyo wauliza kutenda.

*Walitafuta kuwa kama yeye walipojaribu kuzielewa njia zake.*

## TABIA HIZI ZILIKUWA GANI?

1. **Imani**
   Walimuamini. ***"Mwanzo huo wa ishara Yesu aliufanya huko Kana ya Galiraya, akaudhihirisha utukufu wake, nao wanafunzi wake wakamuamini"*** **Yohana 2:11.**
   Imani ni tabia muhimu ya wanafunzi. Wakati Petro alipo mtambua Yesu alikuwana imani kubwa ya kutembea baharini. Alipo yaondoa macho yake kwa Yesu akaanguka Ila bado alikuwa na imani ya kulilia Yesu kwa msaada **Mt 14:25-31.**

2. **Kuabudu**
   Katika maisha yao wanafunzi walimuabudu Yesu. ***"Nao waliokuwamo ndani ya chombo wakamshujudia wakisema, hakika wewe umwana wa Mungu"*** **Mt 14:33**

   ***"Simioni Petro alipoona hayo, alianguka magotini, akasema, ondoka kwangu kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana"*** **Luka 5:8.**

   Baada ya kufufuka kwake, wanafunzi walimuabudu Yesu: ***"Kisha akamuambia Tomaso, Leta hapa kidole chako; uitazame mikono Yangu; ulete na mkono wako uutie umbavuni mwangu; wala usiwe asiye amini bali aaminiye. Tomaso akajibu, akamwambia Bwana wangu na Mungu wangu!"*** **Yohana 20:27-28**

3. **Ufahamu wa maandiko**
   **a.** Waliyajua maandiko na wakakumbuka vile ilikuwa imetabiriwa.
   ***"Wanafunzi wake wakakumbuka yakuwa imeandikwa, wivu wa nyumba yako utanila"*** **Yohana 2:17**
   **b.** ***"Basi alipofufuka katika wafu, wanafunzi wake wakakumbuka alisema hivi, wakaliamini andiko na lile neno alilolinena Yesu"*** **Yohana 2:22**

4. **Waliuliza ufahamu**
   ***"Kisha Yesu akawaaga makutano, akaingia nyumbani; wanafunzi wake wakamwedea, wakasema, tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni"*** **Mt 13:36.**
   Pia katika **Mathayo 15:12-15, Mariko 7:17, Mariko 10:10.**

   Yesu ababanua kati ya wale walioyasikia mafundisho na wanafunzi waliokuja kujifundisha kutoka kwake. ***"Akajibu, akawaambia, ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali hao hawakujaliwa"*** **Mt 13:11**

5. **Walitumia muda peke yao na yeye**
   Yesu aliwaita kando kuwaelezea mambo
   "***Akawaita wanafunzi wake akawaambia…"*** **Mariko 12:43**

***"Lakini akawaeleza wanafunzi wake mwenyewe mambo yote kwa faragha"*** **Mariko 4:34.**

Pia walienda kando peke yao kupumzika. ***"Akawaambia, Njooni ninyi peke yenu kwa faragha, … mkapumzike kidogo"*** **Mariko 6:31**

### 6. Walimfuata yeye

Walipo mfuata (kuambatana) naye waliona jinsi alivyo hudumu, na wakashuhudia nguvu za neno lake na matendo. ***"Akatoka huko, akafika mpaka nchi yakwao; wanafunzi wake wakamfuata"*** **Mariko 6:1**

"***Akaondoka Yesu, akamfuata, pamoja na wanafunzi wake."*** **Mt 9:19**

***"Mwingine wa wanafunzi wake akamwaambia, Bwana, nipe ruhusa kwanza, niende nikamzike baba yangu. Lakini Yesu akamwamwabia, nifuate; wacha wafu wawazike wafu wao. Akapanda chomboni, wanafunzi wake wakamfuata."*** **Mt 8:21-23.**

### 7. Waliomba naye

***"Ikawa alipokuwa akisali kwa faragha, wanafunzi wake walikuwako pamoja naye"*** **Luka 9:18.**

### 8. Walimuuliza yesu awafunze jinsi ya kuomba

***"Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwabia, Bwana, tufundishe sisi kusali, kama vile Yohana aliwafundisha wanafunzi wake."*** **Luka 11:1**

Kama jawabu la ombi hili Yesu ametupatia 'mfano wa Maombi' ambayo yajulikana kwetu kama ombi la Bwana. **(Luka 11:2-4, Mt 6:9-13,)**

### 9. Walikuwa watiifu

Aliwapa changamoto wale waliomwita 'Bwana' ***"Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?"*** **Luka 6:46-47**

Wakati Yesu alimwaambia Simioni atweke kilindini Petro alitii hata kama hakuelewa kwa nini Yesu alimwaambia afanye hivyo.

***"Simoni akajibu akamwabia, Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishuza nyavu."*** **Luka 5:4-5**

# MAJUKUMU YA MWANAFUNZI

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwa mfano. Sasa kupitia neno na Roho anatarajia wanafunzi kufanya kama alivyo fanya.

***"Amin, Amin, nawaambieni, yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya: naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwakuwa mimi naenda kwa Baba"*** **Yohana 14:12**

Katika mwangaza wa mafundisho ya Yesu:

1. **Majukumu yako ni yapi kulingana na neno la Mungu?**
   *(Tizama sehemu ya pili)*

**Soma Yohana 8:31-32**

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

Tafakari haya yana nafasi ipi katika maisha yako

- **a.** Kusoma Biblia
- **b.** Kujifunza Neno
- **c.** Kushiliki ufunuo/ufahamu wako kutoka kwa Neno
- **d.** Kufundisha wengine Neno

Jitafakali katika mwangaza wa **Mathayo 24:45.** Utapokea Baraka za **aya 46?**

2. **Yesu alisema maombi yaliyojibiwa ni ishara ya mwanafunzi wa kweli**
   (*Tazama sehemu ya tatu*)

**Soma: Yohana 15:7**
Tafakari maisha yako ya maombi katika mwangaza wa **Mathayo 6:9-13**

- **a.** Wahisi Mungu uombapo? Unawasiliana nayeye kama Baba yako?
- **b.** Una ufahamu yakuwa yeye yuko katika enzi ya mbinguni unapo omba?
- **c.** Ni rahisi kufuata muundo alioupatiana Yesu katika ombi hili?
- **d.** Unahabari yakuwa anafahamu mahitaji yako na ana suluhisho kwa maombi yako yote?

Unafuatilia kiwango gani?

Ni mambo yapi yana kipaumbele unapoomba?

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

3. **Yesu alisema kupenda na kutumika kama alivyofanya ni ishara ya mwanafunzi wa kweli**
   (*Tazama sehemu ya nne*)

**Soma Yohana 13:35**

Una uwezo kiasi gani kuwafanyia wengine mambo ya upendo – bila kujizuia na kufanya kama ni kitu cha lazima?

Unayaona mahitaji ya wengine na kujaribu kukutana nayo uwezapo?

Unayajua aliyoyajua Yesu alipo waosha wanafunzi wake miguu? **Yahana 13:3**

**a.** ______________________________________________________________

**b.** ______________________________________________________________

**c.** ______________________________________________________________

4. **Tafakari maisha yako katika mwili** (*Tazama sehemu ya tano)*

**Soma: Luke 14:27**

Unakufa kila siku?

Ni mambo yapi yako sawa ndani ya maisha yako kama matokeo ya ubatizo? **Warumi 6:2-14**

**a.** ___________________________________________________________

**b.** ______________________________________________________________

**c.** ______________________________________________________________

**d.** ______________________________________________________________

Unaishi namna gani katika maisha mapya kama matokeo ya ubatizo wa maji?

Wawezaje kusema kwa urahisi yakuwa hautawaliwi na mambo kwa njia yoyote? **Waphilipi 3:7-9.**

5. **Anafahamu kikamilifu mamlaka uliyonayo katika Kristo?**
   (*Tazama sehemu ya saba*)

**Soma: Luka 10:19-20**

Mamlaka haya yanakusaidia kufanya nini?

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

6. **Unatembeaje vyema katika kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu?**
   (*Tazama sehemu ya nane)*

**Soma Matendo ya mitume 1:5,8.**

Kusudu la kimsingi la nguvu hizi ni nini? **Mdo 1:8**

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

*Yesu aliwafunza wanafunzi wake kwa mfano, Sasa kupitia neno na Roho anatarajia wanafunzi wake wafanye kama alivyotenda.*

***"Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba"*** **John 14:12**

## *7.* Umefaya nini na 'talanta' uliopewa?

**Soma Mathayo 25:14-30.**

__________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________

Kimaombi tafakari yafuatayo. Chukuwa muda kutafakari juu ya mambo haya na changamoto.

- Pokea himizo ambayo mtume Paulo alinena kwa Timotheo katika, **2Timotheo 2:2**
  **"*Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine"***

- Hakikisha unatembea katika kazi ambazo Bwana alikuandalia kabla ya msingi wa ulimwengu.
  ***"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea mwanzo Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo"*** **Efe 2:10.**

- ***"Iangalie sana huduma ile uliopewa katika Bwana, ili uitimize"*** **Kol 4:17**

- Hebu ***"Tusimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu"*** **Kol 4:12b**

- ***"Hebu Kristo aumbike ndani yenu"*** **Gal 4:19**

# KUTUMWA ULIMWENGUNI KAMA KRISTO ALIVYOTUMWA

Yesu aliwafunza wanafunzi wake na akawatuma ulimwenguni kama naye alibvyotumwa. Aliwaombea haswa kwa wale aliowatuma.

***"Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo ninawatuma hao ulimwenguni"*** **Yohana 17:18**. Yesu alipanua maombi haya kwa wale ***"Watakaoniamini kwa sababu ya neno lao"*** **Yohana 17:20.**

Yesu tayari alikuwa ameongea na Baba juu ya kazi alizokuwa ametenda katika kuwatayarisha wanafunzi hawa ili watimize kazi yao hapa ulimwenguni **Yohana 17:1-14.** Aliomba pia Yesu asiwatoe hapa ulimenguni, bali ***"Awalinde na Yule muovu"*** **(aya 15)**

Kabla ya kuwatuma alimuuliza Baba **"*Awatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli"*** **(aya 17)**. Hakikisho yake ni ***"Na kwa ajiri yao najiweka wakfu mwenyewe, ili nao watakaswe katika kweli*** **(aya 19).**

Kisha Yesu anahusisha wote: ***"Watakao amini kwa sababu ya neno lao"*** **(aya 20)** Ili waamini wote wawe ***"Na umoja; kama wewe, Baba ulivyo ndani yangu…Ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma"*** **(aya 21)**

*Hivyo Yesu anawatuma wote wanao amini ulimwenguni,*
*wawe mmoja na Baba kama vile yeye alivyo mmoja na Baba.*

## YESU ALITUMWA KWA SABABU GANI?

### Yesu alitumwa kutimiza unabii

**a)** Atakuwa **Mungu pamoja nasi**
**Isaya 7:14** Inatabiri bikira atamzaa Mwana ambaye jina lake ataitwa Imanueli, hivyo ni, ***'Mungu pamoja nasi'***

**b)** Atazaliwa **kwa Roho**
Malaika akamhakikishia Yusufu, aliye mpoza bikira Maria ***"Mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu"*** **Mt 1:20.**

**c)** Hatima yake ni **kuleta wokovu**
**"*Yeye ndiye atakaye waokoa watu wake kwa dhambi zao."*** **Mt.1:21**

**d)** Atakuwa **Mtawala na Mchungaji mwema**
**Mika 5:2** Anatabiri yakuwa kutoka Bethlehemu ***"Kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakaye kuwa mtawala katika Israeli"*** **Mt 2:6.**

- Katika kujaribiwa kwake mbele ya Pilato Yesu alitambua **Haki yake ya kutawala** aliposema: ***"Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nilikuja ulimwenguni, ili nishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu"*** **Yohana 18:37.**

- Alihubiri nafasi yake kama **Muchungaji mwema** ambaye ***"Atoaye uhai wake kwa ajiri ya kondoo"*** **Yohana 10:11** na anasema: ***"Nawajua walio wangu, nao walio wangu wanijua mimi"*** **aya 14.**

**e)** Alikuja awe **nuru** kwa ulimwengu wa giza
**Isaya 9:2** Anatabiri juu ya nuru kubwa itokayo wajia watu wa mataifa. Yohana anamfunua Yesu kama uhai utokao leta nuru kwa watu **Yohana 1:4.** Yohana pia anaongea juu ya giza ambayo haikutambua nuru (**aya 5).**

**f)** Isaya alitabiri yakuwa atakuja kama **mtumishi wa Mungu**
**Isaya 42:1-8** inamueleza yeye na jukumu lake kwa watu wa Mungu kama mtumishi wa Mungu. Atakuwa agano la Mungu kwa watu wake **(aya 6)**. Katika **Mdo 3:26,** Petero anadhibitisha kwamba. ***"Mungu, akisha kumfufua mtumishi wakeYesu, alimtuma kwenu kwanza, ili kuwabarikia kwa kuwaepusha kila mmoja wenu na maovu yake."***

Mtume Paulo anaongea kuhusu Yesu katika utumishi wake na anawahimiza waamini wote ***"Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayoilikuwamo ndani ya Kristo Yesu" Wafilipi 2:5-8***

Yesu alionyesha wajibu wake kama mtumishi wakati aliwatawadha wanafunzi wake miguu (**Yohana 13:3-5).** Kisha akawaamuru wanafunzi wake kupendana kwa njia hio kama ishara ya wanafunzi wake kweli **aya 34-35**

## YESU ALITUMWA NAMNA GANI?

### 1. Yesu alitumwa kumwakirisha Baba

Mtume Paulo, katika kuongea juu ya siri hii, anaandika: **"Mungu alidhihirishwa katika mwili" 1 Timotheo 3:16.** *Mungu alikuja ulimwenguni katika mfano wa mwanadamu na akaitwa YESU.*

Wakati Tomaso na Philipo walimuhoji Yesu, aliwajibu vyema: ***"Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba" Yohana 14:7.***
***"Aliye niona mimi amemuona Baba" Yohana 14:9.***
***"Hausadiki kuwa mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu" Yohana 14:10.***

Yesu anawaambia wanafunzi wake ya kuwa utukufu wa Mungu u ndani yake. ***"Sasa ametukuzwa Mwana wa Adamu, naye Mungu ametukuzwa ndani yake, Mungu naye ametukuzwa ndani ya nafsi yake; naye ametukuzwa mara"*** **Yohana 13:31-32.**

### 2. Yesu alitumwa amtii Baba – hata kifo cha msalaba

Alikubali jukumu alilopewa na akatambua ya kuwa ni lazima atimize wajibu huu ***"Imenipasa kufanya kazi zake yeye aliyenipeleka"*** **Yohana 9:4.**

***"Kama sitazitenda kazi za Baba yangu, msiniamini; lakini nikizitenda, ijapokua hamniamini mimi, ziaminini zile kazi; mpate kujua na kufahamu yakuwa Baba yu ndani yangu, nami ni ndani ya Baba."*** **Yohana 10:37-38**.

**"*Yesu akamwambia, chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikamalize kazi yake"*** **Yohana 4:34.**

***"Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo analiona Baba analitenda; kwamaana yote ayatendayo yeye ndiyo ayatendayo Mwana vile vile"*** **Yohana 5:19.**

**Kazi hizi ni gani?**

a. **Kujenga kanisa (Mt 16:18)** kwa kuwafundisha mitume na wanafunzi ambao "Wangeenda" na kufanya mapenzi Yake.

b. **Kudhihirisha ufalme wa Mungu**
Matendo yake na mafundisho yake zilikuwa zikionyesha watu asili ya ufalme wa Mungu na tabia za Mfalme.

Nimpango wake kwamba ufalme udhihirishwe kupitia kanisa ambalo alitoa uhai wake kwa ajiri yake **Efe 5:25-27.**

Hii ndio kazi ambayo wanafunzi wametumwa wafanye.
Yesu aliwatuma wanafunzi wake ulimwenguni
***"Kama vile Baba alinituma"*** Kutimiza kazi yake.

**WANAFUNZI WANATUMWA KUTIMIZA UNABII WA AGANO JIPYA.**

**A.** Wanafunzi wanatakiwa **kudhihirisha uwepo wa Mungu (Mt 28:20**) kwa "kufanya kazi nizifanyazo" **Yohana 14:12.**

**B.** Wanafunzi wamezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu **kuona** na **kuingia** ufalme wa Mungu **Yohana 3:3-6.**

**C.** Wanafunzi wanatakiwa Kuhubiri injiri ya wokovu ***"Kwaba mataifa yote wahubiriwe kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhabi"*** **Luka 24:47.**

*Hatuwezi kufanya-tena yale Yesu aliye Masihi alitenda, lakini tunabeba Roho wake kupitia Kuzaliwa upya kiroho. Roho wake ndani yetu anatufanya upya (**Mdo 1:8)** kumshuhudia Yesu na kufanya ishara "**zinazo wafuata waamini**" **Mariko 16:17-18.***

**D.** Wanafunzi wanastahili **Kutawala na kutamalaki na mamlaka ambayo Yesu ameweka juu yao, Mt 28:18-20,** kwa maana ***"ametufanya makuhani na wafalme kwa Mungu wake na Baba"*** **Ufu 1:6.**

Yesu aliwapa wanafunzi wake mamlaka ***"Juu ya nguvu zote za adui"*** Kwa msaada ***"wala hukuna kitu kitakachowadhuru"*** **Luka 10:19.**
Anaongezea: ***"Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni"*** **(aya 20)**. Inaonyesha kuwa Yesu, ***"Kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu"*** **Ebr 12:2.**

Wakati Yesu alisema "***Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka"*** **Yohana 9:4.** Alikuwa akionyesha juu ya majukumu aliyokuwa nayo ya kumtii Baba yake.
Kumtii Baba yake ilimpa furaha na anaomba furaha hiyo hiyo iwe na wanafunzi wake **Yohana 17:13.**

**E.** Wanafunzi wanatakiwa **kuwa wachungaji wa kundi ambalo Mungu anaweka chini ya ulinzi wao.**
***"Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari"*** **1 Petro 5:2**. Yesu alimtuma Petro, yule aliyempa funguo za ufalme **Mt 16:19,** ku ***"lisha wana kondoo - wangu, chunga kondoo zangu na lisha kondoo zangu"*** **Yohana 21:15-17.**

**F.** Wanafunzi wanatumwa wawe **nuru kwa ulimwengu wa giza.**

***"Ninyi ni nuru ya ulimwengu"* Mt 5:14**

***"Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.* (aya 16)**

**G.** Wanafunzi wanatakiwa kuwa **watumishi kwa wale wanao watumikia Flp 2:5-8.**

Wakati Yesu aliwatawadha wanafunzi wake miguu aliwaambia wafanye vivyo hivyo **Yohana 13:34-35.**

Yesu aliwatumikia wanafunzi wake kwa njia hiyo ***"Yesu, hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mikononi mwake, nayakuwa alitoka kwa Mungu naye anakwenda kwa Mungu"* Yohana 13:3.**

Sio bidii kwa mwaamini kutumika akiwa na uhakika kuwa mamlaka tuliyopewa (ulidhi wetu), mwanzo wetu wa kiroho na hatima yetu.

## KUFAHAMU MAMLAKA AMBAYO YESU AMETUPA

- **Mamlaka inapatianwa na Mungu**

Alipo watuma wale sabini, Yesu aliwapa wanafunzi wake mamlaka.

***"Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za Yule adui"* Luka 10:19-20.**

Baada ya kifo kufufuka Yesu aliwaambia wanafunzi wake yakuwa alikuwa na mamlaka yote mbinguni na duniani. Kisha akawapa amri ya kueneda na kufanya wanafunzi **Mt 28:18-19**

- **Ni mamlaka ya kiufalme**

Kuzaliwa kiroho kwa mwanafunzi, au kuzaliwa mara ya pili, inatoka kwa Mungu (**Yohana 1:13)** na inapatiana kiingilio katika ufalme wa Mungu kama Mwana wa Mungu (**Yohana3:3-6)**

Mwanafunzi anajua ***"nilipo mimi, nanyi mwepo"* Yohana 14:3.** Yesu ameandaa mahali kwetu tuwe naye milele. Pahali petu pa milele pa kudumu ni kama ***"Mrithi wa Mungu kupitia Kristo"* Gal 4:7.** Anatawala na kutamalaki milele na Mungu ***"Ametufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu"* Efe 2:6.**

Wakati mwanafunzi anafahamu uridhi huu kama mwana wa Mungu anaweza kuwatumikia watu. Anaweza kutembea katika wajibu huu kwa sababu ya kazi ya Kristo msalabani. ***"Yeye asiye jua dhabi alimfanya kuwa dhabi kwa ajiri yenu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye"* 2 Kor 5:21.**

Kubadilishana huku (kuoshwa) katika msalaba inamwezesha mwanafunzi kutembea kama yule "***Amefananishwa na mfano wa Mwana"* (Warumi 8:29).** "***Kufanya kazi kubwa"* (Yohana 14:12)** Yale Yesu aliahidi tutafanya kwa maana tumetiwa Nguvu na Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu.

- **Ni mamlaka yenye Baraka**

**"*Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema … Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu"* Efe 2:4-6.**

***"Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki na Baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho."* Efe 1:3.**

## KUTUMWA

### ➢ Kumpokea Yesu

Yesu ametuahidi ya kuwa kama mwanafunzi ambaye Yesu ametuma amepokelewa, wale wanaompokea mwanafunzi huyo watakuwa wanampokea Yeye na aliyemtuma Yeye!
***"Amin, amin, nawaambieni, yeye ampokeaye mtu ye yote nimpelekaye, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenipeleka."*** **Yohana 13:20.**

### ➢ Yesu atadhihirishwa

Wakati Yesu alipowatuma wanafunzi, aliwatuma "***watangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe"*** **Luka 10:1.** Hii ni lazima itendeke kwa kila mmoja aliyetumwa'. Mwanafunzi anaweza tarajia ya kuwa Yesu atadhihirisha uwepo wake katika kila hali kila mahali ambapo ametumwa kwa kuwa kutumwa ni kwa nguvu za Roho Mtakatifu **Mdo 1:8**

### ➢ Upendo wa Mungu atadhihirishwa

Ni kwa sababu ***"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwana pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye.*** **Yohana 3:16-17.**

Katika waraka wake, Yohana anatukumbusha juu ya upendo wa Mungu ambao ulimfanya amtume Mwana wake ulimwenguni na anaongezea ***"Kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi katika ulimwenguni humu"*** **1 Yohana 4:17**

Kama Yesu alivyotumwa na Baba kufunua upendo na mapenzi ya Baba vivyo anawatuma wanafunzi ulimwenguni waujulishe upendo wake na mapenzi yake.

***"Kama vile ulinituma mimi ulimwenguni,***
***nami vivyo hivyo niliwatuma hao ulimwenguni"*** **Yohana 17:18**

***"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mikiwabatiza,***
***kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu;***
***na kuwafundisha kushika yote niliyo waamuru ninyi;***
***na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dhahari"***
**Mathayo 28:19-20**

# KUMTIA NGUVU MWANAFUNZI

1. **Maombi**

   Tumeona ya kuwa maombi yalio jibiwa ni kuonyeshwa kwa nguvu za Mungu katika huduma ya mwanafunzi. Katika kumbukumbu ya wanafunzi kushindwa kumtoa pepo kutoka kwa kijana, Yesu aliongeza kufunga ikiwa jambo la muhimu sana la kutia nguvu katika hali (**Mariko 9:29)**

2. **Kutumwa**

   Katika **Luka 10:1-20** Yesu aliwatuma wanafunzi sabini wawili kwa wawili ***"Watangulie kwenda mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe."*** **(aya 1)** Anawaambia chakufanya na cha kusema (**aya 9**)

   *Kutumwa na Yesu na kutii kwa mwanafunzi matokeo ni furaha mwanafunzi anapoona nguvu za Mungu zikifanya kazi kakika huduma yake.* **(aya 17-19)**

3. **Kupewa mamlaka**

   Baada ya tukio hili, Yesu aliwapa mamlaka ya kudhihirisha nguvu zake.
   "***Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za Yule adui wala hakuna kitu kitakachowadhuru"*** **Luka 10:19.**
   Kisha anawakumbusha mambo makubwa ya kufanya. "***Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni"*** **(20)**

4. **Ahadi ya Roho Mtakatifu**

   Wakati Yesu alipokuwa akisema juu ya kifo na kutoeka kwake aliwaahidi wanafunzi wake yakuwa hatawaacha wakiwa yatima. "***Naja kwenu"*** **Yohana 14:18**
   Alifunza juu ya Roho Mtakatifu atakayedumu ndani yao ambaye atakuwa:
   "***Msaidizi mwingine"*** **Yohana 14:16,**
   ***"Akaaye nanyi hata milele"*** **16,**
   ***"Ndiye Roho wa kwel" maana "Anakaa kwenu"*** **aya 17**

   Yesu anaahidi kujidhihirisha kwa yule anampenda na anamtii: **Yohana 14:21**
   Roho Mtakatifu atawafundisha na kuwakumbusha wanafunzi mafundisho yake**: 26**
   **Yohana 15:25-27,** na **Yohana 16:7-15** Inapatiana ahadi zingine za kazi ya Roho Mtakatifu za kuwapa nguvu wanafunzi.

5. **Katika kupaa kwake Yesu aliwapa wanafunzi wake maagizo:**

   **Lk 24:49 "*Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu".*** Twasoma kuhusu ahadi ya Baba katika **Ezekieli 36:26-28.**

   Luka anarudia amri hii kungojea ubatizo wa Roho Mtakatifu katika **Mdo 1:5.**

   Matokeo ingekuwa "***Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi yote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi"*** **Mdo 1:8.**

Neno *"shahidi"* yamaanisha mfia dini. Kwa hivyo kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu atawezesha mwanafunzi kujifia na kumpa nguvu za kumshuhudia Yesu.

Wanafunzi **walipotii** na **kungojea katika maombi** walipokea utimilifu wa ahadi za Yesu. Kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa jia kuu katika siku ya Pentekote iliwapa nguvu wanafunzi **Mdo 2:4** na wakaona kuzaliwa kwa kanisa la Yesu Kristo **Mdo 2:41.**

Kitabu cha matendo ya mitume kinathihirisha wanafunzi (na mitume):

- Wakidumu katika neno
- Wakienda mahali walipotumwa
- Wakihubiri injiri bila uoga
- Wakipokea jawabu za maombi
- Wakiona na kuhisi uthihirisho wa nguvu za Bwana
- Wakihesabu kila kitu bule ili wampate Kristo
- Wakiyatoa maisha yao ili wawaokoe wengine

***"Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu;***
***lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu"***
***Lk 24:49***

# MAAGIZO YA MWANAFUNZI

***"Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake;***

***lihubiri neno, uwe tayari, wakati ufaao na wakati usiokufaa,***

***shawishi, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho"***

**2 Tim 4:1-2**

***"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli"***

**2 Tim 2:15**

**AMINA.**